# MUNGU NA VIUMBE HAI

FABIAN BENJAMIN

Mwanadamu ameumbwa kwa namna ya ajabu na ya kutisha. Kwa usanifu wa Mwumbaji, mazingira yalitengenezwa vyema kwa ajili ya maisha ya mwanadamu. Akapewa jukumu la kuwatawala viumbe wa baharini, angani na nchi kavu. Kupitia uelewa huu wa kutawala na kutiisha, wengi wamekuwa na maisha mazuri ya kiuchumi, kiroho, kijamii na kimwili.

Maendeleo makubwa yameonekana katika uso wa dunia kutokana na matumizi sahihi ya maarifa aliyojaliwa mwanadamu. Uvumbuzi ukizidi kila wakati na kurahisisha mfumo wa maisha, vyombo vya usafiri katika anga, nchi kavu na majini vimekuwa msaada mkubwa kukimbiza kasi ya maendeleo kwa jamii na taifa.

Wengi waliochukua muda wao katika kitabu cha asili, wamevumbua vitu vingi sana katika uso wa dunia. Walipata mazingira tulivu, akili zao zikafikiri kwa kina zaidi wakiwa kwenye anga hewa safi ya miti ya asili, kila jawabu la maswali yenye utata lilipatikana. Maarifa yao yalidumu kuongezeka kwa kadiri walivyojifunza zaidi.

Nyimbo tamu za ndege wa angani asubuhi mapema kunapokucha, zinatukumbusha kutafuta maarifa miguuni pa Mwokozi wetu ili kuwahi katika majukumu tukiwa salama chini ya uongozi wa Mungu; tunapaswa kutoa shukurani kwa kila jambo litakalotendeka siku hii maana tulianza na Bwana.

Anga likiachia nuru angavu, jua likianza kumulika dunia, ni kumbukumbu ya utii wa viumbe wa Mungu katika utendaji, tangu alipotamka mianga mikubwa miwili kuwapo; jua kutawala mchana na mwezi kutawala usiku. Havijawahi kufanya mgomo bali hutekeleza wajibu kama Bwana alivyosema. Jua huleta mwanga unaovutia kwa mimea, tukitazama miti inavyopendeza wakati upepo mwanana ukipuliza na matawi yake kucheza-cheza kwa mwendo wa madaa. Nani asiyetamani kukaa chini ya jua la asubuhi lililotamu kwa ngozi, huku akipata utulivu chini ya mti mzuri na upepo ukipuliza kwa ustarabu.

Kumbukumbu zinaturejea juu ya viumbe alivyoviumba Mungu, upole wa njiwa siku zote huburudisha moyo, utulivu wa kondoo unafurahisha akili, juhudi ya chungu inakaza misuli yetu tayari kwa kujituma, uhodari na ujasiri wa simba unatusogeza katika ushindi ndani ya pambano la maisha ya utafutaji, maono ya tai yanatunyanyua juu ya vikwazo na dhoruba na utambuzi wa nyuki kwa harufu ya maua inatufanya tukumbuke kutumia muda vizuri na kutokupoteza nguvu katika utendaji usio na manufaa maishani.

Hakika ni raha na furaha kujifunza kuhusu viumbe wa asili. Utapata mbinu zote za maisha katika uhai aliokujalia Mungu; hutakariri njia moja ya utafutaji, huwezi kukata tamaa na kamwe hutakosa fursa maishani. Jifunze daima, utaona mabadiliko makubwa mno maishani.